JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA MAJI

# HUDUMA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

## MWONGOZO KUHUSU UUNDAJI NA USAJILI WA KISHERIA WA VYOMBO VYA WATUMIAJI MAJI VIJIJINI

## (ESTABLISHMENT AND REGISTRATION OF LEGAL COMMUNITY OWNED WATER SUPPLY ORGANISATIONS)

**Aprili, 2010**

# YALIYOMO

**1. UTANGULIZI............................................................................................................ 3**

1.1 Sera ya Maji.................................................................................................................. 3

1.2 Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Sekta ya Maji.................................................... 3

1.3 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.................................................................... 3

1.4 Vyombo vya Watumiaji Maji......................................................................................... 4

1.5 Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na.12 ya Mwaka 2009..................................... 4

1.6 Kanuni za Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji....................................................... 5

**2. UUNDAJI NA USAJILI WA VYOMBO VYA WATUMIAJI MAJI...................................... 5**

2.1 Uundaji wa Vyombo vya Watumiaji Maji....................................................................... 5

2.2 Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji......................................................................... 6

2.3 Makabidhiano ya Cheti.................................................................................................. 7

**3. MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI KATIKA UUNDAJI NA USAJILI WA VYOMBO VYA WATUMIAJI MAJI KISHERIA.......................................... 7**

3.1 Majukumu ya Kamati ya Muda ya Chombo cha Watumiaji Maji................................... 7

3.2 Uchaguzi wa Kamati ya Kudumu ya Chombo cha Watumiaji Maji............................... 8

3.3 Majukumu ya Kamati ya Utendaji.................................................................................. 8

3.4 Majukumu ya Viongozi wa Chombo cha Watumiaji Maji.............................................. 9

3.5 Majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kata/ Afisa Mtendaji wa Kijiji................................. 10

3.6 Majukumu ya Msajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji................................................ 10

3.7 Majukumu ya Halmashauri za Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji...................................... 10

3.8 Majukumu ya Serikali Kuu............................................................................................ 11

**4. HITIMISHO.................................................................................................................. 12**

# WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

## MWONGOZO KUHUSU UUNDAJI NA USAJILI WA KISHERIA WA VYOMBO VYA WATUMIAJI MAJI VIJIJINI (ESTABLISHMENT AND REGISTRATION OF LEGAL COMMUNITY OWNED WATER SUPPLY ORGANISATIONS)

## 1. UTANGULIZI

Kwa muda mrefu huduma ya maji kwenye miradi ya maji iliyoko vijijini imekuwa ikiendelea kupungua na mahali pengine miradi kutofanya kazi kabisa kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo kutosimamiwa vizuri na kukosa matengenezo muhimu. Katika baadhi ya maeneo, watumiaji wa maji wengine bado wana dhana kuwa jukumu la kuwapatia wananchi huduma ya maji ni la Serikali pekee, kama ilivyokuwa hapo awali. Aidha, katika baadhi ya maeneo, kuna mwamko usioridhisha kwa watumiaji maji kuchangia katika gharama za ujenzi na uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji. Upungufu huo umesababisha kuhitajika kwa mpango thabiti na endelevu wa uratibu na usimamizi wa utoaji wa huduma hii katika ngazi za kitaifa, mkoa na wilaya. Serikali imeandaa sera na mkakati utakaowezesha majukumu mbalimbali kutekelezwa katika ngazi husika.

### 1.1 Sera ya Maji

Kwa kuzingatia kuwa maji ni bidhaa yenye gharama na inahitaji kulipiwa, Sera ya Maji ya mwaka 2002 inasisitiza ushirikishaji wa watumiaji wa maji katika ngazi zote katika kuandaa, kugharamia ujenzi, kuendesha na kutengeneza miradi ya maji kwa kutumia fedha zinazokusanywa kutokana na mauzo ya maji. Aidha, sera inaagiza uundaji wa vyombo vya watumiaji maji, ambavyo vitahusisha wadau mbalimbali . Vyombo hivi vitakuwa na maamuzi kuhusu mipango na shughuli za upanuzi, uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji. Kuhusu maeneo ya vijijini, sera inaelekeza kuwa bei ya maji itosheleze gharama za uendeshaji na matengenezo ya mradi. Bei ya maji vijijini haitajumuisha gharama za uwekezaji (*depreciation*).

Hapo awali, mchakato wa usajili wa vyombo vya watumiaji maji ulikuwa ukisimamiwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Hata hivyo, imebainika kuwa mchakato huo ulikuwa unachukua muda mrefu kutokana na urasimu katika taratibu za usajili. Katika kuondoa urasimu huo, serikali imefanya marekebisho katika usajili wa vyombo hivyo kupitia Sheria ya Maji Na.12 ya mwaka 2009. Mabadiliko hayo yamezipa Halmashauri za Wilaya, Mji, Manispaa na Majiji mamlaka ya kuteua msajili na kusimamia mchakato mzima wa usajili chini ya Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na.12 ya mwaka 2009, iliyoanza kutumika rasmi tarehe 1.8.2009.

### 1.2 Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Sekta ya Maji

Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Sekta ya Maji unaelekeza jinsi sera ya maji ya mwaka 2002 itakavyotekelezwa na kufafanua kuhusu muundo ya kitaasisi na kisheria ili kuwezesha mambo muhimu yaliyoainishwa katika mkakati kutekelezwa kwa ufasaha.
Kwa kuzingatia mfumo wa kitaasisi uliokubalika katika mkakati, vyombo vya watumiaji maji vya jamii [Community Owned Water Supply Organisation-(COWSO's)] vinatambulika kisheria kuwa vina jukumu la kumiliki, kusimamia, kuendesha na kuhudumia miradi ya maji vijijini kwa niaba ya jamii.

### 1.3 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

Ili kutekeleza sera, mwaka 2006 Serikali iliandaa na kupitisha Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Maji. Miongoni mwa mambo muhimu katika mkakati ni pamoja na yafuatayo: (i) vyombo vya watumiaji maji viundwe na kusajiliwa kisheria ili kudumisha huduma ya maji; (ii) jamii maskini izingatiwe katika utoaji

wa huduma ya maji; (iii) usafi wa mazingira ujumuishwe katika utoaji wa huduma ya maji; (iv) teknolojia sahihi itumike katika utoaji wa huduma ya maji; (v) sekta binafsi ishirikishwe katika utoaji wa huduma ya maji; na (vi) ukarabati na upanuzi wa miradi iliyopo upewe kipaumbele.

Kufuatia kukamilika kwa sera ya maji na mkakati wake, mwaka 2006 Serikali iliandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, programu itakayoongoza upatikanaji wa huduma endelevu ya maji na usafi wa mazingira kwa wakazi wa vijijini na mijini. Utekelezaji wa programu hiyo unalenga katika kukidhi matakwa na misingi ya sera ya maji ya mwaka 2002.

Programu hii inahusu ujenzi wa miundombinu ya maji vijijini, uhamasishaji wa wananchi kuhusu usafi wa mazingira vijijini, na uimarishaji wa Halmashauri na taasisi mbalimbali. Utekelezaji wa programu unahusisha taasisi mbalimbali, zikiwa katika ngazi ya taifa, mikoa, Halmashauri, vijiji, na sekta binafsi. Ngazi ya taifa inatoa miongozo ya utekelezaji, kufuatilia na kuratibu utekelezaji. Ngazi ya mkoa inafuatilia na kutoa ushauri kwenye Halmashauri. Ngazi ya Halmashauri ndio nguzo kuu ya utekelezaji.

### 1.4 Vyombo vya Watumiaji Maji

Vyombo hivi vinaweza kuundwa kisheria katika mifumo mbalimbali ikiwemo: vikundi vya watumiaji maji, jumuiya za watumiaji maji, bodi za wadhamini, vyama vya ushirika, mashirika yasiyo ya kiserikali, makampuni, n.k. ingawa jumuiya za watumiaji maji zinahamasishwa kutumika zaidi katika ngazi za Halmashauri. Vyombo hivi vinatarajiwa kusimamia na kugharamia shughuli zote za kuendesha na kuhudumia miradi ya maji na kuhakikisha kuwa miradi ya maji inajiendesha kwa kutumia fedha za makusanyo.

Hivyo basi kupitia Sheria Na. 12 ya 2009, Halmashauri zote ambazo hazijaunda vyombo vya kisheria vya kusimamia uendeshaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijini zitasimamia uundaji vyombo vya watumiaji maji kwa kufuata kanuni pamoja na mwongozo huu. Aidha, vijiji ambavyo tayari vilishaanza mchakato wa uundaji wa vyombo hivyo na viko katika hatua mbalimbali vinatakiwa kukamilisha zoezi hili kwa kutumia mwongozo huu mpya.

Wahandisi wa Maji wa Wilaya kwa kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya watasimamia uundaji wa vyombo vya watumiaji maji kwa kushirikiana na Wahandisi wa Maji katika Sekretarieti za Mikoa, ambao ndio washauri na watafsiri sera ya maji katika ngazi ya mkoa.

### 1.5 Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na.12 ya Mwaka 2009

Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira kifungu Na. 31(1), jumuiya za watumiaji maji zinaundwa kwa makubaliano baina ya wananchi walio wengi katika eneo husika. Jumuiya zitakazoundwa kwa mujibu wa sheria hii kupitia kifungu Na.31(1), zitasajiliwa chini ya kifungu Na.34 cha sheria Na.12 ya 2009. Vyombo vingine vilivyoundwa kupitia sheria nyingine vitahusika pia na usajili chini ya sheria hii. Vyombo hivyo pamoja na vile vilivyotajwa kwenye kifungu namba 31(2) na 62(2) ni (i) Jumuiya ya Watumiaji wa Maji (Water Consumers Association); (ii) Udhamini; (iii) Vyama vya Ushirika; (iv) Kampuni; (v) Taasisi zisizokuwa za Kiserikali na (vi) Vyombo vingine kama vitakavyoidhinishwa na Waziri mwenye dhamana.

Vyombo vilivyopo pamoja na vile vitakavyoundwa vitahusika na kutambuliwa na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na.12 ya mwaka 2009 kama ilivyofafanuliwa kwenye kifungu Na.62. Kifungu hiki kinataka vyombo vyote vilivyosajiliwa, ikiwa pamoja na vile vilivyosajiliwa chini ya sheria nyingine viwasilishe katiba na randama za makubaliano yao kwa Msajili aliye katika Halmashauri ya Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji husika, ili viweze kusajiliwa chini ya kifungu Na. 34 cha sheria Na. 12 ya 2009.

### 1.6 Kanuni za Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji

Kanuni za usajili wa vyombo vya watumiaji maji, zimeandaliwa chini ya kifungu 34(1) cha sheria Na.12 ya Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009. Kanuni za Maji na Usafi wa Mazingira (usajili wa vyombo vya kijamii vya watumiaji maji) za mwaka 2009, zilitangazwa katika gazeti la serikali Na. 21, la tarehe 22.1.2010. Kanuni hizi na tafsiri zake zinataja uteuzi wa msajili wa vyombo vya watumiaji maji katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji. Pia, zinaainisha majukumu ya wadau mbalimbali ambao wanahusika katika uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji vinavyomilikiwa na wananchi wenyewe.

Aidha, kupitia katika kanuni, mwongozo huu pia unaainisha taratibu mbalimbali za kufuatwa katika hatua za uundaji, usajili, pingamizi, rufaa na pia hatua za kufuatwa katika kusitisha au kufuta hati za usajili.

## 2. UUNDAJI NA USAJILI WA VYOMBO VYA WATUMIAJI MAJI

### 2.1 UUNDAJI WA VYOMBO VYA WATUMIAJI MAJI

Ufuatao ni mwongozo kuhusu uundaji wa vyombo vya watumiaji maji:

(i) Uongozi wa kijiji kupitia kamati yake ya maji na usafi wa mazingira ya kijiji au kamati ya maji kwa kushirikiana na Wataalam Washauri au Timu ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Wilaya utaitisha kikao cha awali kati ya viongozi wa kijiji na kamati ya maji na usafi wa mazingira ya kijiji ili kuuza wazo la kuunda chombo cha watumiaji maji kwa miradi iliyokwishakamilika, inayoendelea kujengwa au itakayojengwa.

(ii) Uongozi wa kijiji na kamati ya maji na usafi wa mazingira ya kijiji wataafikiana kuhusu kuunda chombo cha watumiaji maji na uamuzi huo utawasilishwa kwenye mkutano mkuu wa kijiji.

(iii) Washauri au Timu ya Wataalam wa Maji na Usafi wa Mazingira ya Wilaya wataelimisha wananchi kuhusu aina mbalimbali za vyombo vya watumiaji maji, taratibu na hatua za usajili kwa kila aina ya chombo, umuhimu wa kuunda vyombo vya watumiaji maji vilivyosajiliwa kisheria na kuwaongoza na kutoa ushauri katika mchakato wa kuchagua aina ya chombo wanachokipenda. Chombo cha watumiaji maji kitaanzishwa baada ya wananchi kukubaliana kwa pamoja kwa kuzingatia masharti au vigezo vinavyotawala katika aina ya chombo kilichochaguliwa.

(iv) Serikali ya Kijiji itaitisha mkutano wa wanakijiji wote *(village assembly)* ili kuamua kwa pamoja kuunda na kusajili aina ya chombo cha watumiaji maji wanachoona kinawafaa kwa mujibu wa maelekezo ya wataalam wa wilaya. Mkutano huo utateua kamati ya muda kwa kuzingatia usawa wa kijinsia itakayosimamia uundaji na usajili wa chombo cha watumiaji maji.

(v) Kamati hiyo itaandaa rasimu ya katiba na kanuni za chombo kilichopendekezwa. Kwa mujibu wa mwongozo huu uandaaji wa rasimu ya katiba na kanuni utamshirikisha Mwanasheria wa Halmashauri husika.

(vi) Kamati ya muda iliyoteuliwa itawasilisha rasimu ya katiba na kanuni kwenye mkutano wa kijiji *(village assembly)* ili kujadiliwa na kupitishwa na mkutano huo.

(vii) Kamati ya muda itawasilisha rasimu ya katiba na kanuni kwenye kikao cha maendeleo ya kata ili kuthibitisha kutokuwepo kwa pingamizi ndani ya kata na kupata ridhaa. Hii itawezesha kubaini kuwepo au kutokuwepo kwa jumuiya kama ile inayopendekezwa.

(viii) Baada ya kupitishwa kwa rasimu za katiba na kanuni, Mwenyekiti na Katibu wa kamati ya muda na Mwenyekiti na Katibu wa Serikali ya Kijiji, kwa pamoja watawasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri rasimu ya katiba, kanuni na nyaraka zote zinazotakiwa kwa ajili ya uundaji wa chombo cha watumiaji maji, ili kipate ridhaa ya Halmashauri. Mkurugenzi wa Halmashauri ana uhuru wa kufanya ukaguzi au uchunguzi wowote anaouhitaji kupitia wataalam wake ili kujua hali halisi, kabla ya kuwasilisha ombi la kuunda chombo kwenye kamati au vikao husika kwa ajili ya kupata ridhaa.

(ix) Mkurugenzi wa Halmashauri atawasilisha rasimu ya katiba na kanuni kwenye kikao cha timu ya Menejimenti ya Halmashauri, kikao cha Kamati ya Huduma za Jamii ya Halmashauri na Baraza la Madiwani, ili kuridhia uundaji wa chombo cha watumiaji maji.

(x) Mkurugenzi wa Halmashauri ataiandikia barua kamati ya muda kupitia Serikali ya Kijiji husika, akionyesha kuwa Halmashauri imetoa ridhaa ya kuundwa kwa chombo husika katika kijiji kilichowasilisha maombi hayo.

(xi) Kufikia hatua hii, chombo cha watumiaji maji tayari kitakuwa kimeundwa kulingana na katiba na kanuni walizojiwekea.

## 2.2 USAJILI WA VYOMBO VYA WATUMIAJI MAJI

(i) Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri itaandika barua ya utambulisho wa chombo cha watumiaji maji ambacho maombi yake yamefuzu vigezo vinavyotakiwa kwenda kwa msajili wa chombo cha watumiaji maji.

(ii) Kamati ya muda iliyoteuliwa na wananchi itaandaa na kuwasilisha barua ya maombi ya kusajili chombo cha watumiaji maji kwenda kwa Msajili kupitia kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji na Afisa Mtendaji wa Kata, ikiambatanisha katiba na kanuni ya chombo hicho na muhtasari wa mkutano mkuu wa kijiji pamoja na majina ya wajumbe waliohudhuria na sahihi zao na barua husika kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri inayoonyesha kuwa Halmashauri imeridhia uundaji wa chombo hicho.

(iii) Waombaji wa usajili wa chombo cha watumiaji maji watajaza fomu ya maelezo iliyotayarishwa na msajili ambaye ameteuliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Manispaa, Mji au Jiji.

(iv) Waombaji watalipia ada ya usajili kama itakavyopangwa na Msajili.

(v) Msajili ataunda kamati ya kuhakiki maombi ya usajili wa chombo cha watumiaji maji katika eneo husika. Pale ambapo itabidi, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ihusishwe kama itakavyoonekana kuwa inafaa.

(vi) Msajili atahakiki uhalali wa chombo cha watumiaji maji kilichofuzu vigezo vilivyotakiwa kwenye usajili na kutoa mapendekezo au ushauri kwa chombo ambacho hakikufuzu ili kiweze kufuzu.

(vii) Wananchi watafahamishwa kuhusu matokeo ya uhakiki iwapo maombi yao yanafuzu vigezo vilivyowekwa au kama yanahitaji maboresho kabla ya kusajiliwa.

(viii) Msajili atatoa hati ya kisheria ya usajili kwa chombo cha watumiaji maji kilichofuzu vigezo vilivyotakiwa ili kitambulike kisheria na kuweza kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa kwa mujibu wa sheria.

(ix) Baada ya usajili kukamilika, Msajili ataendelea na hatua ya kutangaza chombo alichokisajili katika Gazeti la Serikali ili kutambuliwa rasmi.

### 2.3 MAKABIDHIANO YA CHETI

Baada ya taratibu za usajili kukamilika, Msajili atakabidhi cheti kwa Kamati ya Kudumu mbele ya Timu ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Wilaya na kisha kamati ya kudumu itaonyesha cheti hicho kwa wananchi wa eneo husika kwenye mkutano wa hadhara.

Katika mkutano huu ndipo kamati ya muda itakabidhi shughuli na nyaraka zote za uendeshaji wa chombo cha watumiaji maji kwa kamati ya kudumu ya chombo hicho. Shughuli za kamati ya muda zitakoma katika hatua hii.

## 3. MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI KATIKA UUNDAJI NA USAJILI WA VYOMBO VYA WATUMIAJI MAJI KISHERIA

### 3.1 Majukumu ya Kamati ya Muda ya Chombo cha Watumiaji Maji

Ili kuwezesha mchakato wa uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji kisheria kufanyika mapema, Kamati za Maji na Usafi wa Mazingira zilizopo katika vijiji, zitachukua jukumu la kamati ya muda katika kipindi chote cha mchakato wa uundaji na usajili. Pale ambapo kuna mgogoro na kamati iliyopo, kamati ya muda itachaguliwa upya na wananchi.

Majukumu ya kamati ya muda ni pamoja na:

(i) Kuwezesha uandaaji wa rasimu ya katiba ya chombo cha watumiaji maji kwa mujibu wa mwongozo chini ya usaidizi wa Mwanasheria watakayemchagua. Mwanasheria huyo anaweza kutoka kwenye maeneo yafuatayo:

- Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji
- Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
- Sekta binafsi/Mwanasheria wa kujitegemea

(ii) Baada ya kamati ya muda kukamilisha rasimu ya katiba na kanuni, itaitisha mkutano wa wanakijiji wote ili kuzijadili na kuzipitisha. *Mkutano huu utatakiwa uandaliwe, ukiwa na muhtasari wenye majina ya wajumbe waliohudhuria ambayo yameandikwa kwa mkono na kusainiwa na wajumbe wenyewe binafsi.* Baada ya hapo kamati itaandaa nakala nne za barua ya maombi. Nakala moja itabaki kwa kamati ya muda, nyingine zitaipelekwa kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji, Afisa Mtendaji wa Kata na nyingine kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Nyaraka zifuatazo zitaambatanishwa kwenye barua:

- Katiba na Kanuni za chombo kilichopitishwa na wananchi
- Fomu Na.1 kutoka kwenye kanuni za uandikishaji wa vyombo vya watumiaji maji (pamoja na ada ya usajili ya chombo cha watumiaji maji).
- Orodha ya majina ya wanachama iliyoandikwa kwa mkono na kusainiwa.
- Muhtasari wa mkutano wa wanachama walioamua kuunda chombo, uliotiwa saini na Mwenyekiti na Katibu wa kamati ya muda.
- Muhtasari wa mkutano wa wanachama walioamua kupitisha katiba ya kudumu ya chombo cha watumiaji maji na kanuni zake. Wasifu (CV) wa viongozi wakuu wa kamati ya kudumu, Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina.

(iii) Kamati ya muda pia itaandaa na kusimamia taratibu za uchaguzi wa viongozi wa chombo cha watumiaji maji kitakachopendekezwa na jamii. Miongoni mwa sifa za msingi za viongozi wa chombo cha watumiaji maji ni pamoja na hizi zifuatazo:

- Awe anajua kusoma na kuandika kwa ufasaha, na umri zaidi ya miaka 18
- Awe ni mkazi wa eneo husika kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu
- Awe ni mtu mwaminifu na ambaye hajapata kushtakiwa kwa makosa ya jinai.
- Kamati ya muda na Serikali ya Kijiji inaweza pia kuweka sifa nyingine kadri itakavyoona inafaa na kukubalika katika jamii.

### 3.2 Uchaguzi wa Kamati ya Kudumu ya Chombo cha Watumiaji Maji

Kamati ya muda ya chombo cha watumiaji maji na Serikali ya Kijiji, itatangaza nafasi 3 za uongozi wa juu na nafasi 5 za wajumbe wa kamati ya kudumu. Uchambuzi wa waombaji wa nafasi za uongozi katika Kamati ya Kudumu ya chombo cha watumiaji maji utafanyika kwa kushirikisha Serikali ya Kijiji chini ya usimamizi wa wawakilishi wa Halmashauri ya Wilaya, Manispaa, Mji au Jiji.

Kamati ya kudumu ya chombo cha watumiaji maji itachaguliwa baada ya kukamilika kwa hatua ya uundaji wa chombo cha watumiaji maji, na Mkurugenzi wa Halmashauri kutoa barua ya ridhaa ya uundaji wa chombo hicho.

Uchaguzi wa viongozi utazingatia uwakilishi wa wanawake katika nafasi za juu, ili angalau viongozi wanawake wawe asilimia 50 au zaidi. Majina ya viongozi waliochaguliwa ili kuendesha chombo hicho baada ya kusajiliwa yatatumwa kwa msajili wa vyombo vya watumiaji maji.

Baada ya shughuli zote za uundaji na usajili wa chombo cha watumiaji maji kukamilika, kamati ya muda itakabidhi shughuli zote za utendaji kwa viongozi waliochaguliwa rasmi na kuunda uongozi wa chombo cha watumiaji maji wa eneo husika.

### 3.3 Majukumu ya Kamati ya Utendaji

Kila chombo kitakuwa na kamati ya utendaji kulingana na aina ya chombo kilichoundwa na kusajiliwa. Kamati hiyo itakuwa na wajibu wa kufanya kazi zifuatazo:

(i) Kuhakikisha utoaji wa huduma ya maji safi, salama na ya kutosha kama ilivyoelekezwa kulingana na viwango vya ubora wa maji vya kitaifa na kimataifa.
(ii) Kuendesha shughuli zote za vyombo vya watumiaji maji kwa uangalifu mkubwa, kuendeleza na kutunza vifaa vya miradi ya maji kwenye maeneo yote ambayo vyombo vya watumiaji maji vinatoa huduma.
(iii) Kuendeleza na kulinda matumizi mazuri ya maji kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo.
(iv) Kuelimisha na kuwapa wananchi taarifa za mapato na matumizi, ambao kwao ndio sababu ya kuundwa kwa vyombo hivi vya watumiaji maji, pamoja na taarifa kuhusu elimu ya afya na utunzaji salama wa maji.
(v) Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa ambavyo vyombo vya watumiaji maji vinaona ni muhimu kwa watu wanaotumia maji.
(vi) Kukusanya fedha za malipo ya maji kutoka kwa watumiaji wa maji na kuzitumia kwenye kuendesha, kutengeneza na kuendeleza miradi ya maji.
(vii) Kutoa taarifa kwa uongozi wa jumuiya ya watumiaji maji kuhusu shughuli zote kubwa zinazofanyika katika vyanzo ambazo zinaweza kuathiri utoaji wa huduma ya maji.

(viii) Kuandaa na kutoa taarifa za nusu mwaka na mwaka kwa jumuiya ya watumiaji maji na nakala kutumwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.
(ix) Chombo cha watumiaji maji kitaweka utaratibu unaofaa wa kutoa kiwango mahsusi cha huduma ya bure ya maji kwa watu wasiojiweza wanaoishi kwenye jamii husika. Ni vema watu wasiojiweza watambuliwe na Serikali ya Kijiji na taarifa hiyo kuwasilishwa kwa maandishi kwa chombo cha watumiaji maji.
(x) Kuhudhuria katika mikutano ya kiserikali inayoandaliwa kwenye ngazi ya Halmashauri inayowahusu na katika maeneo ya miradi ya maji.
(xi) Kuratibu bajeti za vyombo vya watumiaji maji ili zihuishwe katika bajeti ya serikali ya kijiji.
(xii) Kutatua migogoro itakayojitokeza kwenye chombo cha watumiaji maji.

### 3.4 Majukumu ya Viongozi wa Chombo cha Watumiaji Maji

Kila chombo cha watumiaji maji kitakuwa na viongozi wake waliochaguliwa kidemokrasia kwa kushirikisha watumiaji wa maji katika eneo husika. Miongoni mwa majukumu ya viongozi hawa ni pamoja na kufanya kazi zifuatazo:

(i) Kufanya uchambuzi na kuthibitisha mapendekezo ya bei za maji ambazo zitaviwezesha vyombo vya watumiaji maji kuendelea kutoa huduma nzuri ya maji, bila kuathiri kundi lolote la watumiaji maji.
(ii) Kuishauri Serikali katika utungaji wa sera inayohusiana na maendeleo na utunzaji wa vyanzo vya maji.
(iii) Kuandaa mipango na kusimamia utekelezaji wa miradi mipya ya maji.
(iv) Kuwasiliana na vyombo vya watumiaji maji vingine kuhusu masuala ya maji, utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya upanuzi wa shughuli za maji.
(v) Kuhamasisha ujenzi, utunzaji na matumizi bora ya vyoo, elimu ya afya na usafi wa mazingira.
(vi) Kuhakikisha kunakuwa na uhusiano mzuri kati ya asasi mbalimbali na vyombo vingine vya watumiaji maji kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji.
(vii) Kusimamia utunzaji wa mazingira katika eneo ambalo vyombo hivi vinahudumia ili kusitokee uchafuzi.
(viii) Kuendeleza shughuli zote zilizokuwa zinafanywa na Halmashauri kupitia Idara yake ya Maji katika maeneo yao kabla ya kuanzishwa vyombo vya watumiaji maji.
(ix) Kuunda kamati mbalimbali na kuzikabidhi majukumu ya shughuli za vyombo vya watumiaji maji.
(x) Kupendekeza sheria ndogo zinazohusiana na maji na utoaji wa huduma ya maji na kupeleka mapendekezo kwa Mkurugenzi kwa Halmashauri kwa hatua zaidi.
(xi) Kupitisha ratiba ya kazi za vyombo vya watumiaji maji.
(xii) Kuidhinisha utoaji wa huduma au vifaa vinavyohusiana na shughuli za huduma ya maji kama itakavyoelekezwa na Halmashauri kutoka kwa vyombo vya watumiaji wa maji kwenda kwa vyombo vingine vya watumiaji maji.
(xiii) Kupokea na kutekeleza maagizo ya Mkurugenzi wa Halmashauri kuhusu masuala ya kawaida au maalumu, yanayohusiana na uendeshaji wa vyombo vya watumiaji maji.
(xiv) Kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya bei za maji na gharama nyingine kwa huduma zinazotolewa na vyombo vya watumiaji maji kwa Halmashauri.
(xv) Kutoa miongozo kwa kamati mbalimbali za utekelezaji kuhusu hatua zinazohitajika au zinazofaa katika kuwezesha utoaji mzuri wa huduma ya maji na matengenezo katika njia endelevu.
(xvi) Kutoa miongozo kwa kamati mbalimbali za chombo cha watumiaji maji kuhusu mipango ya uwekezaji kwenye programu za muda mrefu, kati na mfupi na uandaaji wa bajeti za mwaka za vyombo vya watumiaji maji.
(xvii) Kuandaa miongozo kuhusu utunzaji wa fedha na taarifa za utendaji kazi wa vyombo vya watumiaji maji.

(xviii) Kuandaa miongozo kwa vyombo vya watumiaji maji kuhusiana na maendeleo ya wafanyakazi.
(xix) Kuandaa miongozo kwa watendaji kuhusu utawala wa vyombo vya watumiaji maji.

### 3.5 Majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kata/Afisa Mtendaji wa Kijiji

Kwa kuzingatia kuwa Afisa Mtendaji wa Kata/Afisa Mtendaji wa Kijiji ni msimamizi mkuu wa shughuli zote za maendeleo na pia mlinzi wa amani katika eneo husika anatakiwa kuhakikisha kuwa katiba iliyokubaliwa kutumika na chombo cha watumiaji maji inatekelezwa ikiwa ni pamoja na kuhakiki mambo yafuatayo:

(i) Endapo chombo kinachoombewa usajili kimeundwa kwa kufuata taratibu na miongozo iliyowekwa.
(ii) Endapo uamuzi wa kuunda chombo hicho ni wa wananchi wenyewe, bila kushurutishwa na wala si maamuzi ya kikundi cha watu wachache wenye malengo binafsi.
(iii) Kuhakiki uandishi wa katiba kama umefuata utaratibu ulioambatanishwa *(rejea katiba ya mfano Na.1 iliyoambatanishwa).*
(iv) Kuhakiki kama chombo cha watumiaji maji kipo na ni pekee katika eneo husika, na hakuna mwingiliano na chombo kingine.
(v) Kushiriki katika hatua za tathmini ya waombaji wa uongozi ili kuthibitisha kuwa waombaji wana ridhaa ya jamii husika.
(vi) Shughuli za utoaji wa huduma ya maji zinazofanywa zinahusiana na mahitaji na malengo yaliyotajwa na si vinginevyo.
(vii) Kutatua migogoro yoyote itakayojitokeza wakati wa uundaji, usajili na uendeshaji wa chombo cha watumiaji maji.

### 3.6 Majukumu ya Msajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji

Sheria ya Maji inamtaka Msajili aliyeteuliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji kusajili vyombo vyote vya watumiaji maji *(registration of COWSO's)* katika eneo husika. Pamoja na majukumu ya msingi yaliyoko katika kanuni, msajili wa vyombo vya watumiaji maji atatekeleza yafuatayo:

(i) Kupokea barua ya utambulisho wa chombo cha watumiaji maji kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji iliyoambatana na maombi ya kusajili chombo cha watumiaji maji katika eneo la Halmashauri husika, yaliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kata, Afisa Mtendaji wa Kijiji, na kutoka katika chombo kinachokusudiwa kusajiliwa au kutoka kwenye chombo kingine kilichoidhinishwa ama kusajiliwa kisheria kwa sheria nyinginezo za nchi, ili kiweze kutekeleza majukumu yake kisheria.
(ii) Kuhakikisha kama viambatanisho vyote vinavyohitajika kwenye maombi ya usajili wa chombo hicho cha watumiaji maji vipo na ni halisi/halali kutumika katika usajili.
(iii) Kutoa mapendekezo na ushauri unaopaswa kufuatwa kuhusiana na usajili wa vyombo vya watumiaji maji ambavyo havikufuzu usajili, ili yaweze kufanyiwa marekebisho na pale ambapo imeshindikana kueleza sababu.
(iv) Kusajili vyombo vyote vinavyojihusisha na utoaji wa huduma za maji kwenye Halmashauri husika, vilivyoanzishwa chini ya sheria nyingine zilizopewa madaraka ya kuvisajili kama vyombo vya watumiaji maji kulingana na Sheria ya Maji Na. 12 ya mwaka 2009.
(v) Kusajili kisheria vyombo vya watumiaji maji ambavyo vinavyofuzu vigezo vinavyotakiwa kwenye usajili.

### 3.7 Majukumu ya Halmashauri za Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji

Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji ndiyo msimamizi *(regulator)* wa vyombo vya watumiaji maji. Majukumu yake makuu ni kama ifuatavyo:

(i) Kuteua Msajili wa vyombo vya watumiaji maji vitakavyofanya kazi chini ya Sheria hii
(ii) Kutoa fidia kwa wote watakaoharibiwa mali zao wakati wa upanuzi wa shughuli za maji.
(iii)Kutoa ruzuku kwa vyombo vya watumiaji maji kwa kazi muhimu za kupanua na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma ya maji.
(iv)Kusaidia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kulipia madeni ambayo vyombo vya watumiaji maji vitakuwa vinaidai Serikali na taasisi zake.
(v) Kusaidia upatikanaji wa ruzuku kwa ajili ya kulipia gharama zinazodaiwa na Serikali na taasisi zake, kwa mfano, umeme, madawa, n.k.
(vi)Kuteua afisa/maafisa watakaoratibu shughuli za uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji na usafi wa mazingira, katika vijiji vyenye vyombo vya watumiaji maji vilivyoko katika maeneo yao.
(vii) Kumshauri Waziri wa Maji na Umwagiliaji kuhusu utendaji wa vyombo vya watumiaji maji vilivyoko katika maeneo yao.
(viii) Kutoa miongozo kwa vyombo vya watumiaji maji kuhusiana na utekelezaji wa masuala yote yanayohusu makubaliano/mkataba kati ya vyombo vya watumiaji maji na taasisi au chombo kingine.
(ix)Kusimamia mchakato wa maandalizi ya kuunda vyombo vya watumiaji maji pamoja na kusimamia/kuwezesha uchaguzi wa kamati za muda, kamati ya kudumu na kuwasilisha mapendekezo kwa msajili, kufanya mapitio ya kuwezesha kuridhia usajili. *(Jukumu hili linafanyika kwa kuzingatia kijitabu cha mwongozo wa uwezeshaji jamii, katika uanzishaji wa vyombo vya watumiaji maji kilichotolewa na Wizara ya Maji mwezi Septemba 2006 na kusambazwa katika Halmashauri zote nchini).*
(x) Kufanya upekuzi wa waombaji kuthibitisha kuwa waombaji ni kikundi kinachokubalika humu nchini, na kwenye jamii husika.
(xi) Kuridhia mapendekezo ya bei za maji zilizopendekezwa na vyombo vya watumiaji maji.
(xii) Kuhamasisha utoaji wa huduma ya usafi wa mazingira kwenye maeneo yanayozunguka miradi ya maji.
(xiii) Kutoa ushauri na kushirikiana na serikali ya kijiji au taasisi yeyote inyohusika na ardhi ili kupanga matumizi ya ardhi katika maeneo ya karibu na miradi ya maji.
(xiv) Kutoa msaada wa kitaalam kwa kikundi kinachokusudia kuanzisha na kusajili chombo cha watumiaji maji endapo utahitajika.
(xv) Kutoa na kuwasilisha Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ratiba ya uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji na nakala za taarifa za vyombo vya watumiaji maji vilivyosajiliwa kisheria katika maeneo yao, kila robo mwaka.
(xvi) Kupatia ufumbuzi na kusuluhisha migogoro ya aina yoyote itakayojitokeza baina ya wananchi na vyombo vya watumiaji vilivyoko katika maeneo yao.

### 3.8 Majukumu ya Serikali Kuu
(i) Kufanya mapitio ya sera ya maji pale inapohitajika.
(ii) Kutoa mwongozo wa jinsi ya kuunda kusajili, kusimamia na kuongoza vyombo vya watumiaji maji kwa ushirikiano na Halmashauri za Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji.
(iii)Kusimamia na kuratibu utunzaji na hifadhi ya vyanzo vya maji na usafi wa mazingira.
(iv)Kuratibu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kusaidia kuvijengea uwezo vyombo vya watumiaji maji.
(v) Kuratibu na kutoa misaada ya kiufundi na kifedha, kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa miradi ya maji na usafi wa mazingira.
(vi)Kuratibu utoaji wa mafunzo ya kudumu kwa maafisa wa miradi ya maji na usafi wa mazingira inayomilikiwa na vyombo vya watumiaji maji vijijini.

## 4. HITIMISHO

Ili miradi ya maji iwe endelevu na iweze kutoa huduma ya maji kwa ufanisi ni lazima iwe na fedha za kujiendesha zitakazotokana na mauzo ya maji. Hii itawezesha huduma ya maji kuwa endelevu. Sera ya maji inasisitiza miradi ijengwe, iendeshwe na kusimamiwa na wananchi ili ijiendeshe kwa kufanya matengenezo kila inapohitajika bila kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

Kila mradi wa maji ulioko kijijini ni lazima usajili kisheria chombo cha watumiaji maji kitakachoendesha mradi huo. Lengo kuu la kuanzisha vyombo vya watumiaji maji ni kuifanya miradi imilikiwe na kusimamiwa na wananchi wenyewe ili kuhakikisha kuwa huduma ya maji inakuwa endelevu.